# Kuanza…anza kuota

Kitabu cha Mwanzo, huanza na Mungu akiangalia ulimwengu aliouumba ukiwa na machafuko. Hata hivvyo, hatujaelezwa ni kwa nini Mungu hakutosheleka na vile kulivyokuwa na hii ilikuwa ni fursa yake ya kutazamia siku bora. Wakati fulani sisi sote hujikuta tumekumbwa na haja yakubadilisha jambo katika maisha yetu ama ulimwengu wetu. Nyakati hizi hutupa fursa za kutilia maanani na kukumbatia ndoto mapya, ambayo ndiyo ndoto ya Mungu kwa siku zetu za usoni.

Unapochunguza maisha yako na uone eneo linalohitaji kuangaliwa kwa umakini utafute mwelekeo wa Mungu na uanze kuwazia……. Tafakari kile kingelikuwa badala ya kile kilichoko na ukumbuke yote yawezekana na Mungu**.**

**Ombi la leo** Baba wa mbinguni, ni hamasishe na ndoto zako katika maisha yangu na unifanye kama ulivyo wewe.niwezeshe kuondoa viwango ambavyo nimeweka katika maisha yangu na uandike tena mipaka yangu ili uwezo ulioumba ndani yangu upate nafasi. Fungulia tafakari zangu na unikomboe kutokana na hofu zote.

**Maandiko ya leo** zaburi 126:1 Bwana alipowarejeza mateka wa Sayuni, tulikuwa kama waotao ndoto.

Ayubu 33: 14-16 Kwa kuwa Mungu hunena mara moja, naam hata mara ya pili, ajapokuwa mtu hajali. Katika maono ya usiku, usingizi mzito uwajiliapo watu, katika usingizi kitandani.Ndipo huyafahamu masikio ya watu, nakuyatia muhuri mafundisho yao.

# Ndoto sio mpango

Ndoto sio mpango. Mungu alipotazama ulimwengu uliokuwa na giza, katika kitabu cha Mwanzo 1:2, roho ya Mungu ikatulia juu ya uso wa maji, kuchukua mda unaofaa kukuza mpango.

Maisha yetu hayajatengenezwa kuwa {hifadhi ya barafu) kuhifadhi kazi za kale za Mungu, ila yawe hifadhi za joto za kukunza matendo ya Mungu ya usoni. Hii hali inajulikana Kama kutafakari.Hatua ya kwanza, ni kujua unachohitaji kubadilisha.Lazima uwe na mpango kujua jinsi ya kubadilisha. Ota ndoto za Mungu katika maisha yako,na uanze kukuza mipango na kumpa Mungu mda na fursa akuhamasishe. Endelea kuwakilisha ndoto yako kwa Mungu katika maombi na umpe nafasi akuongoze hatua inayofuata.

**Ombi la leo** Ewe Bwana, nataka kufaulu katika ndoto zako maishani mwangu. Njenga mpango ndani yangu na unipe kila hatua. Naamua kukupa wewe mawazo yangu na kuelekeza nia yangu yote Kwako.

**Maandiko ya leo** Mithali 3:5-6 Mtumaini Bwana kwa moyo wako wote, wala usizitegemee akili zako mwenyewe; katika njia zako zote mkiri yeye, naye atanyosha mapito yako.

**Joshua 1:8** Kitabu hiki cha torati kisiondoke kinywani mwako, mbali yatafakali maneno yake mchana na usiku, upate kuangalia kutenda sawasawa na maneno yote yaliyoandikwa humo; maana ndipo utakapo ifanikisha njia yako, kisha ndipo utakapositawi sana.

# *Tangaza Ndoto*

Katika kitabu cha Mwanzo, Mungu aliota ya kwamba siku moja dunia haitakuwa katika giza. Akaangalia njia zake zote na akakuza mpango wake lakini alifaulu baada ya kuchukua hatua ya kwanza na kusema,"Iwe nuru." Mungu akatamka ndoto yake na kisha akatangazia ulimwengu ya kwamba mambo yatabadilika. Tunapohitaji mabadiliko na kupokea mpango wa Mungu uliohamasishwa, tunaweza kuanza mabidiliko hayo kwa tamko la imani na kutangaza kwa ulimwengu mambo yatakuwa tofauti. Yesu anatuagiza tunenee milima yetu kwa imani. Hakuna linalobadilika kwa sababu ya ndoto ambazo tukonazo ama mipango ya kubadilisha. Mungu ameagiza ulimwengu nakuuamuru kutii kwa tamko lako la imani. Anza kutamka ndoto yako kwa imani.

***Ombi la leo*** Ewe Bwana, fanya ulimi wangu chombo chako na unene mapenzi yako yatendeke kunipitia mimi. Weka mlinzi kwa kinywa changu na ulinde milango ya midomo yangu . Tumia maneno yangu kuleta uhai kulingana na mapenzi yako katika jina la Yesu.

***Maandiko ya leo:*** Ayubu 22:28 Nawe utakusudia neno nalo litathibitika kwako, na mwanga utaziangazia njia zako.

Zaburi: 2:7 Nitaihubiri amri.

Marko 11:23 Amini, nawaambia, yeyote atakayeuambia mlima huu, ng'oka ukatupwe baharini, wala asione shaka moyoni kwake, ila aamini kwamba hayo asemayo yametukia, yatakuwa yake.

# *Uamuzi mbaya, uamuzi usio faa, na makosa yanayo tugharimu ni sehemu ya utaratibu lakini sio shida*

Maisha yana uamuzi mwingi, mwingine ni wasawa na mwingine ni wa gharama na mbaya. Hata wakati tumefanya uamuzi usiofaa, Mungu hata hivyo, huwa pamoja na sisi. Kinacho onekana kama kuteleza kwetu huenda ikawa ni fursa ambayo Mungu alikuwa akitafuta ili atufunze na atusongeshe mbele katika kiwango cha juu maishani.

Wakati mwingine, kile kinacho onekana kana kwamba ni uamuzi mbaya, uamuzi usio faa, ama kosa linalotugharimu, huenda ikawa sio kosa la makusudi ila, ni sehemu ya hatua ambazo Mungu atatumia kukuunda, kukuhami, na kukuandaa vyema kwa siku yako ya ushindi. Ni vyema tung'ang'ane ili tujifunze kutokana na makosa yetu na tutarajie Mungu ayatumie kwa njia moja ama nyingine kwa manufaa yake mwenyewe.

*Ombi la leo :* Mungu,nataka kuona mambo jinsi unavyoyaona. Nifunze kutoshushwa moyo na mambo nisiyoweza kubadilisha. Nipe neema na uniruhusu kujifunza kutokana na makosa niliyotenda ili niweze kuwa wa huduma bora kwako.

***Maandiko ya leo:*** 2 Wakorintho: 4:17-18 maana dhiki yetu ni nyepesi, iliyo ya mda wa kitabo tu, yatufanyia utukufu wa milele uzidio kuwa mwingi sana; tusiviangalie vinavyoonekana, bali visivyoonekana. Kwa maana vinavyoonekana ni vya mda tu; bali visivyoonekanani vya milele.

Kutoka 1: 12: lakini kwa kadiri walivyowatesa ndivyo walivyoongezeka na kuzidi keunea….

Warumi 8:28: Nasi twajua ya kuwa katika mambo yote Mungu hufanya kazi pamoja na wale wampendao katika kuwapatia mema, yaani, wale walioitwa kwa kusudi lake.

## *Twawaza tunavyowaza, twahisi tunavyohisi, na twataka tunavyotaka kwa sababu twaamini tunavyoamini*

Kile kila mmoja wetu anawaza, kile anachohisi, na anachotaka kinatokana na kile anachoamini. Hayo yote ni sawa kama tunaamini kile kilicho sawa. Hata hivyo, wengine wetu wanatawaliwa na hofu isiyoweza kueleweka, matarajio yasiyowezekana, uoga usio na msingi, ama shaka isiyo kubalika. Wengine wame angamizwa na kuamini kwao kwamba hakuna Mungu.

Twawaza tunavyowaza, twahisi tunavyohisi, na twataka tunavyotaka, kwa sababu twaamini tunavyoamini hata wakati kile tunachoamini sio lazima kiwe ni ukweli. Kuna mtihani mmoja tu wa ukweli- neno la Mungu, Bibilia. Maandiko yanasema nini kuhusu maisha yako, wewe mwenyewe, na siku zako za usoni? Tafuta na kisha uanze kuamini. Yape muda na umakini unaohitajika na yataanza kubadilisha jinsi unavyowazia, hisi, na pia, unavyotaka.

*Ombi la Leo:* Baba nifunze neno lako. Nitalificha kwa roho yangu ili nisiweze kufanya dhambi. Ninenee katika andiko na unionyeshe mpango na mawazo yako kuhusu siku zangu za usoni.Nipe neema yakuweka kado hofu zote na makosa. Na chagua kuamini Neno Lako.

*Maandiko ya leo*: Yohana Mtakatifu 17:17; uwatakase kwa ile kweli, neno lako ndiyo kweli.

Zaburi 19:14; maneno ya kinywa change, na mawazo ya moyo wangu, yapate kibali mbele zako, Ee Bwana, Mwamba wangu na Mwokozi wangu.

Marko Mtakatifu 12:24; Yesu akajibu, akawaambia, je hampotei kwa sababu hii, kwa kuwa hamyajui maandiko wala uwezo wa Mungu?”

## *Tunachosema, kitasemwa*

Ni jambo la muhimu kuchunga unachosema kwa vile huwezi kujua ni nani anayekusikiliza kwa sababu ya teknolojia ya dunia ya kisasa. Iwe ni simu ya rununu imesikika na mtu ambaye hakufaa kusikia, ama ni ukuta unaopitisha maneno kimakosa.Mara kwa mara watu hujikuta wakisikiliza mawasiliano ambayo hayakunuiwa masikio yao. Hata hivyo, jambo hili halifai kutushangaza.

Neno la Mungu ni dhahiri: unachosema kitasemwa. Kwa bahati mbaya, maana uliyokusudia kusema mara nyingi hugeuzwa mawasiliano yanaporudiwa. Hii ndiyo sababu ni vyema kutojihusisha na maongeo yasiyofaa ambayo hatungetaka wengine wayasikie. Huenda ikawa sababu hii ndiyo ilimfanya mwimbaji akamuomba Mungu aweke mlinzi kinywani pake na mngojezi mlangoni pa midomo yake. Nini hicho ambacho huwezi kusema ukijua bila shaka kila mtu atasikia?

*Ombi la leo:* Baba, neno lako linasema kwamba kama mtu atajikinga asikasirishane kwa maneno basi dini yake ni kamilifu. Najua ya kwamba ulimi una uwezo wa kuwasha mioto

katika uhusiano na kutenganisha hata marafiki wa dhati. Niwezeshe kuulinda ulimi wangu na uweke mlinzi kinywani pangu.

*Maandiko ya leo:* Mhubiri: 10:20; Usimlaani mfalme, la, hata katika wazo lako; wala usiwalaani wakwasi chumbani mwako; kwa kuwa ndege wa anga ataichukuwa sauti na mwenye mabawa ataitoa habari.

Luke 12:3 Basi yo yote mliosema gizani, yatasikiwa mwangani; na mliyonena sikioni mwa mtu katika vyumba vya ndani, yatahubiriwa juu ya dari.

Zaburi 141:3 Ee Bwana, uweke mlinzi kinywani pangu, mngojezi mlangoni pa midomo yangu

## *Tunachotenda kitagunduliwa*

Mahakama na magereza yamejaa watu ambao wangejua kile wanafanya kitakuja kugunduliwa na watu hawangalifanya. Ni nini walichokuwa wakiwazia? Hata kama hawangejulikana katika maisha haya hawange toroka bila kugunduliwa. Mambo yote yatawekwa wazi labda kwa maisha haya ama katika kiti cha hukumu cha Yesu.

Tunachotenda kitagunduliwa! Huu ndio ukweli. Ujasiri uliyoko ni tusiyafanye mambo ambayo hatuwezi kutaka wengine wayajue. Maandiko ni dhahiri na kile yanacho simamia kinafaa kutudumisha katika njia hii nyembamba na ambayo imenyooka. Mungu pia hutupatia tuzo kwa uwazi kwa matendo mema tuliyofanya kwa siri…anachotenda kitagunduliwa.

*Ombi la leo :* Mungu tafadhali nipe mimi na wengine wapendwa kwangu hisia njema yakutofanya chochote kisichokufurahisha wewe ama kuleta aibu kwa Jina Lako. Nisaidie kukumbuka ya kwamba mimi ni Mkristo na niwajibu wangu kutenda kama Mkristo, kufanya uamuzi wa sawa na haki.

*Maandiko ya leo:* Luka Mtakatifu: 12:2; lakini hakuna neno lilositirika ambalo halitafunuliwa, wala lilofichwa ambalo halitajulikana.

Mathayo mtakatifu 6:4; sadaka yako iwe kwa siri; na baba yako aonaye kwa siri atakujazi.

Waefeso 6:8; mkijua yakuwa kila neno jema alitendalo mtu atapewa lilo hilo na Bwana.

## *Unachoamini kitajaribiwa*

Katika mfano wa mkulima aliyepanda mbegu katika shamba lake,punde ndege wakaja kujaribu kuiba mbegu hizi kutoka shambani. Baadaye, Yesu akiwaelezea wanafunzi wake mfano huu, aliwafunulia ya kwamba mbegu hiyo inawakilisha Neno la Mungu. Shamba ni roho ya mwanadamu ilhali ndege inawakilisha Shetani. Yesu akasema, “Shetani huja punde kuiba lile neno kutoka kwa roho zao.”

Shetani ni adui wetu na atachukua kila fursa kujaribu kile tunachoamini kuhusu Mungu, wema wake, na upendo wake. Tunauona utaratibu huu ulitendeka wakati Iblisi alimnenea Eva shambani la Edeni.  Alimjaribu Eva kupitia kile alochoamini kwamba alikuwa amesema. Eva alianguka mtihani! Utafanya nini unapojaribiwa?

*Ombi la leo:* Baba wa mbinguni, nipe uwezo wakupita kila jaribio la maisha na kuushikilia ukweli ambao nimejifunza kutaka kwa Neno Lako. Usiache nijaribiwe zaidi ya ninavyoweza kustahimili.

*Maandiko ya leo:* Mwanzo 3:1-5; Basi nyoka alikuwa mwerevu kuliko wanyama wote wa mwitu aliowafanya Bwana Mungu. Akamwambia mwanamke, "Ati! Hivi ndivyo alivyosema Mungu, 'Msile matunda ya miti yote ya bustani'?" Mwanamke akamwambia nyoka, "matunda ya miti ya bustanini twaweza kula, lakini matunda ya mti ulio katikati ya bustani Mungu amesema,' Msiyale wala msiyaguse, msije mkafa'." Nyoka akamwambia mwanamke, 'hakika hamtakufa, kwa maana Mungu anajua ya kwamba siku mtakayokula matunda ya mti huo, mtafumbuliwa macho, nanyi mtakuwa kama Mungu, mkijua mema na mabaya."

## ***Tunachokubaliana kuweka tutakipoteza***

Watu wengi wanatabia nzuri na mienendo isiyo na lawama.  Tulifunzwa utotoni ya kwamba, wizi, uwongo, udanganyifu, na mambo kama hayo sio mazuri. Kwa jumla, tabia zetu zinategemea mienendo yetu na, kuongozwa na mambo tunayoyadhamini. Mara kwa mara hali hutulazimisha kukubaliana na mambo ambayo hatuyapendi ili tupate kujinufaisha.

Kuna sheria ya kukubaliana inayosema yakwamba kile mtu anachokubaliana nacho ili kimnufaishe, mwishowe hukipoteza. Cha kushangaza ni kwamba kanuni hii pia hupatikana kwa neno la Bwana. Ili tuwe wakristo, tuhitajika tujikane, tujitwike msalaba wetu nakumfuata Kristo. Kisha tunaelezwa kwamba tukitafuta kufaidisha maisha yetu, tutapoteza. Hatutapata kile tunakusudia kupata kwa kukubaliana na mambo …kitatupata sisi!

*Ombi la leo* Ewe Mungu niwezeshe kuishi katika udhamana wangu….udhamana ambao nimejifunza kutokana na neno lako. Nisaidie kuwa na uwazi kwa yote ninyotenda na nisiwahi kuuza hekima yangu nipate kitu duni cha muda.

Masomo ya leo. Mariko mtakatifu 8:34-35 Akawaita mkutano pamoja na wanafunzi wake akawaambia, Mtu yeyote akitaka kunifuata na ajikane mwenyewe, ajitwike na msalaba wake, anifuate. Kwa kuwa mtu atakaye nafsi yake ataiangamiza, na mtu atakayeiangamiza nafsi yake kwa anjili yangu na kwa anjili ya Injili, huyu ataisalimisha.

Mathayo 16:26 Kwani atafaidiwa nini mtu akiupata ulimwengu wote, na kupata hasara ya nafsi yake? Au mtu atatoa nini badala ya nafsi yake?

## *Wakati tunafanya kile tu tunachoweza kufanya, huenda Mungu hafanyi chochote*

Wakati mwingi sisi huamua kuishi na uwezo wetu tukiogopa kujaribu yale yanayozidi uwezo wetu. Tunasahau kumtumikia Mungu mwenye uwezo wote aliyenena na ulimwengu ukawa na akaiumba dunia kutoka kwa vitu ambavyo havikuwa. Mungu huhusika sana na yasiyowezekana.

Hakuna hata mmoja anayeweza kufanya yale Mungu ametuita kufanya pasipo Yeye kuingilia na njia kubwa. Kutoka kwa Musa kutawanya maji ya bahari ya shamu, kwenda kwa Elia kuita moto taka juu mbinguni, kutoka Petro akipitia juu ya maji, hadi Mariamu akibingirisha jiwe kutoka kaburini alomo lazwa Yesu, sote twahitaji uungiliaji kati wa kiungu. Tukimwamini Mungu, hakuna kisichowezekana.

*Maombi ya leo* Baba Mungu, ninakuhitaji kwa maeneo yote maishani mwangu. Ingia ndani na unitawale. Nitatenda kazi kama kumaanisha kwamba kazi yote inanitegemea mimi, na nitaomba kama kumaanisha maombi yote inakutegemea wewe. Yachukue yale mimi siwezi kufanya, na unipe uwezo wa kuyafanya. Yote, utukufu ni Kwako.

*Masomo ya leo* Mathayo 19:26 Yesu akawakazia macho akawaambia, Kwa wanadaamu hilo haliwezekani; bali kwa Mungu yote yawezekana.

Mariko Mtakatifu 9:23 Yesu akawaambia“Ukiweza! Yote yawezekana kwake aaminiye.”

Mariko Mtakatifu 14:26, Naye akasema, “Abba Baba, mambo yote yawezekana kwako.Niondolee kikombe hiki; ila sio mapenzi yangu lakini Yako Wewe”

## *Mwelekeo haungojei na wala haumtegemei mtu mmoja*

Wakati hali zilimlazimisha Esta kuamua kumwedea Mfalme bila mwaliko ili akawatetee Wayahudi, aling’ang’ana na uoga. Katika hadithi hii banamu yake na aliyekuwa amemsimamia, Moredekai, alimwelekeza kwa ukweli wakudumu. “Kama utaendelea kunyamaza wakati kama huu, msaada na ukombozi wa Wayahudi utakuja kupitia njia ingine; lakini wewe na jamii yake mtaangamizwa. Nani ajuaye? Huenda ulifanyika malikia kwa wakati kama huu tu.”

Mwelekeo haungojei na wala haumtegemei mtu mmoja. Mungu anampango, atafaulu, na tuna nafasi ya kuhusika. Hata hivyo, tukiamua kutohusika, Mungu bado atafaulu, ila tu atamtumia mtu mwingine.

*Ombi la leo*: Ewe Mungu sitaki kupitwa na nyakati za kukutumikia kwa njia kubwa na Baraka ambazo umeumba kwa sababu yangu mimi. Nisaidie nigudue mwito wangu na nisimame nikiwa tayari kutumika wakati unaponiita.

*Masomo ya leo:* Esta 4:14 Kwa maana wewe ukinyamaza kabisa wakati huu, ndipo kutakapowatokea Wayahudi msaada kwa njia nyingine; ila wewe utaangamia pamoja na

mlango wote wa baba yako; walakini ni nani ajuaye kama wewe hukuujia ufalme kwa ajili ya wakati kama huo?

1 Wafalme 18:21 Naye Elia akawakaribia watu wote akanena, “Mtasita-sita katikati ya mawazo mawili hata lini? Bwana akiwa ndiye Mungu, mfuateni; bali akiwa Baali ndiye Mungu, haya! Mfuateni yeye.” Wale watu hawakumjibu neno.

## ***Mbingu na Dunia pamoja huchagua watu wenye bidii, wenye hakiki, na wale wamefanya uamuzi kuongoza vita vyenye ushawishi maishani***

Ulimwengu mzima unamtafuta kiongozi, mtu anayeelewa anapoelekea na anayedhihirisha kuwa anaweza kufaulu. Kama tutawaita, mashupavu, mashujaa, wenye maono, wakiroho ama wenye kutumia nguvu, watu hufuata viongozi kama hao. Ukweli ni kwamba mbingu na dunia huteua watu wenye hakiki, wenye uamuzi, na wenye bidii kuongoza vita vyenye ushawishi maishani. Sisi huweka imani yetu kwa wale wanaoweza kufanya kazi bila kuyumbayumba wanapokutana na hatari. Nini hicho ambacho umeamua kufanya?

*Ombi la leo:* Baba, nisaidie nisiwe mdhaifu ama nizirahi wakati wa matatizo. Nipe maono ya pahali unapotaka niwe na unipe ushupavu wa kukumbana na vikwazo vile vinavyojaribu kunishinda mimi. Nimeamua kuyatimiza mapenzi yako. Nisaidie niongoze wengine wafaulu katika mapenzi yako.

Masomo ya leo: kitabu cha Yoshua 1:9 Je! Si mimi niliyekuamuru? Uwe hodari na moyo wa ushujaa; usiogope wala usifadhaike; kwa kuwa Bwana, Mungu wako, yu pamoja nawe kila uendako.

Kitabu cha Yoshua 1:16-18 wakamjibu Yoshua, wakasema, “Hayo yote uliyotuamuru tutafanya, na kila mahali utakakotutuma tutakwenda. Kama vile tulivyomsikiliza Musa katika mambo yote, ndivyo tutakavyo kusikiliza wewe; Bwana, Mungu wako, na awe pamoja nawe tu, kama alivyokuwa pamoja na Musa. Kila mtu atakayeiasi amri yako, asiyasikilize maneno yako katika mambo yote utakayomwamuru, atauawa. Uwe hodari na moyo wa ushujaa, hilo tu.”

## ***Wacha kuharibu mitaji Kwa matengenezo, sio athari ya utenzi***

Mambo mengi hatufanyi kwa sababu mpya, ila ile ya kawaida. Baadhi ya mitindo hii, tamaduni hizi, ama majukumu haya hayana maana ingine ila ni … tabia za maisha. Mazao yake ni machache, na faida zake ni, kupoteza wakati na rasilimali zingine.

Pengine masaa ni baadhi ya vile vitu vya udhamana. Yakishatumika, hayawezi kupatikana. Kwa hivyo lazima maisha yetu yawajibike. Tunahitaji kujua wakati wakuwacha kupoteza mitaji kwa matengenezo, yanayopeteza wakati na shughuli

zisizokuwa na faida. Jikague mwenyewe na matenzi yako leo, panga majukumu yako na ufurahie amani inayokuja kama matokeo.

Tilia manani……. Ya kwamba Shughuli sio kila wakati zina manufaa.

*Ombi la leo*: Ewe Baba wetu wa mbinguni, naomba unionyeshe mambo yako ya muhimu kwa maisha yangu, wakati wangu,na mitaji yangu. Sitaki kupoteza kipawa chochote cha dhamana kati ya vile umenipea. Nineemeshe kuwacha mambo nisiyoyahitaji na niyabadilishe na yale yazaao matunda katika shani ya maisha yangu.

*Maandiko ya leo:* Tito 3:14 Ni lazima watu wetu wajifunze kuutumia wakati wao katika kutenda mema ili wasaidie katika mahitaji ya kweli, na maisha yao yawe ya kufaa

Waefeso 5:15 Basi, muwe waangalifu jinsi mnavyoishi: Msiishi kama wapumbavu, bali kama wenye hekima.

## *Fuata sauti ya Kwanza wala sio ya Pili*

Kila mtu anastahili maagizo, neno la kibinafsi kutoka kwa Mungu. Ingawa, wakati mwingi watu husikia shuhuda kutoka kwa wengine ambazo ni nzuri na za kusifika, ila hazifuatwi. Kuna utofauti kati ya maelezo jinsi vile Mungu alivyotembea katika maisha ya mtu mwingine na maagizo yanayoeleza vile Mungu angependa kutembea katika maisha yetu. Ni utofauti kati ya sauti ya kwanza na ya pili.

Sauti za pili zinaweza na mara nyingi huwa zinatoka mahali kwingi. Baada ya muda wanafanyika dhaifu na kupungikiwa na nguvu nakunena neno jipya kwao wenyewe. Hata hivyo, sauti ya Mungu, hupeana mwelekeo nakuongeza nguvu kwa kila hali inazozinenea. Muulize akupe masikio ya kusikia sauti, maagizo kwa maisha yako.

*Ombi la leo*: Bwana ulisema ya kwamba kondoo zako husikia sauti yako na kukufuata …kwamba sauti ya mgeni hawatafuata. Nisaidie niwe masikio ya kusikia sauti yako kuu na wazi. Nielekeza kwa ukweli wa Neno Lako ninapomsikiliza Roho wako mtakatifu akininenea mimi binafsi.

*Maandiko ya leo:* zaburi 3:5-6; Mtumaini Bwana kwa moyo wako wote, wala usizitegemee akili zako mwenyewe, katika njia zako zote mkili yeye, naye atayanyosha mapito yako.

Yeremia 33:3; niite, nami nitakuitikia, nami nitakuonyesha mambo makubwa magumu usiyoyajua.

## *Kuna utofauti kati ya kuwa na shida ama kuwa shida*

Wakati sisi kama wakristo tunaingia katika mawazo, mazungumzo, ama vitenzi visivyo wakilisha mtindo wa maisha ya kikiristo, huwa ni shida. Tunapo itambua,tunafaa

kurekebisha. Tusipofanya chochote kuhusu shida tuliyonayo, tunakoma kwa muda Fulani kuwa na hiyo shida, kisha inaanza kutudhuru.

kuna utofauti kati ya kuwa na shida na kuwa shida. Wakati mwingine tibabu ni kuyakubali majukumu yetu ya kibinafsi kwa hiyo shida, nakumuuliza Mungu atusaidie. Wasikilize marafiki wako unao waamini na jamii. Wanaweza wakakusaidia kutambua shida iliyofichika.

*Ombi la leo:* Mungu, niwezeshe kujiona mwenyewe kupitia macho ya marafiki ninao waamini na jamii. Ninee na unipe neema yakushugulikia sehemu za maisha yangu pale ninapowakera wengine,ninapo jipotosha, au ninapo kubatilisha. Nisaidie nisiwahi kujiruhusu kubaki kuwa shida. Nisamehe na unipatie uwezo.

*Maandiko ya leo:* 2 wakorintho 13:5 Jichunguzeni ninyi wenyewe mpate kujua kama kweli mnayo imani. Jichunguzeni ninyi wenyewe. Je, hamjui kwamba Kristo Yesu yumo ndani yenu? Kama sivyo, basi ninyi mmeshindwa.

Luka 6:41-42 Unawezaje kukiona kibanzi kilicho katika jicho la mwenzio, usione boriti iliyo katika jicho lako mwenyewe? Au, unawezaje kumwambia mwenzako, `Ndugu, ngoja nikuondoe kibanzi katika jicho lako,` na huku huioni boriti iliyoko katika jicho lako mwenyewe? Mnafiki wewe! Toa kwanza boriti iliyoko jichoni mwako, na hivyo utaona sawasawa kiasi cha kuweza kuondoa kibanzi kilicho katika jicho la ndugu yako.

## *Uamuzi huhitaji waamuzi*

Inafaa wazazi wawe imara katika uamuzi wao wanapo walea watoto wao katika malezi na kumcha Bwana. Haimaniishi ni sawa, kwamba watoto wengine wameruhusiwa kuwa na tabia mbaya na kujitawala wakiwa wachanga. Wakati mwingi watoto, wanapoathiriwa na wenzao, huona wazazi wanaowajali kama watawala wasiokuwa na haki.

Watu wazima wanaweza pia kuhisi kama wasio tawaliwa kwa haki katika hali zingine za maisha. Watu walio na mamlaka mara nyingine hufanya uamuzi ambao unaweza kuwaumiza wengine.Uhalali wa sauti ya kiongozi unaweza kuonekana na wale wanaofinywa na utawala wake. Hata hivyo, hali zingine zinataka uamuzi wenye ujasiri kutoka kwa viongozi walio halali na ambao wamesimama pahali wanapofaa.

*Ombi la leo:* Ewe Baba, nisaidie niwatambue na kuwafuata viongozi halali ambao Umeniwekea maishani mwangu. Ninapotenda haya Bwana, pia wape neema wale wanaojikuta wakitawaliwa na uamuzi wangu. Naomba wakati wote nikufurahishe, ewe Bwana.

*Masomo ya leo*: Waebrania: 13:17 Watiini viongozi wenu na kushika amri zao; wao huchunga roho zenu usiku na mchana, na watatoa ripoti ya utumishi wao mbele ya Mungu. Kama mkiwatii watafanya kazi zao kwa furaha, la sivyo, watazifanya kwa huzuni, na hiyo haitakuwa na faida kwenu.

Warumi 13:1-2 Kila mtu anapaswa kuwatii wenye mamlaka katika serikali; maana mamlaka yote hutoka kwa Mungu; nao wenye mamlaka wamewekwa na Mungu Anayepinga mamlaka ya viongozi anapinga agizo la Mungu; nao wafanyao hivyo wanajiletea hukumu wenyewe.

## ***Kushindwa hujaribu faradhi yetu, fanaka hujaribu tabia yetu***

Nyakati ngumu, majira mazito,kushushwa moyo, ajali, na kutofaulu hujaribu faradhi yetu. Watu wengi hupitia hali hizi ngumu na kupata fanaka yao maishani. Hata hivyo, maisha hutujaribu mara ya pili ambayo ni ya kuchanga moto sana.

Kushindwa hujaribu faradhi yetu nayo fanaka tabia yetu. Je, tutafanya nini wakati tutakapofaulu maishani na tuwe na muda kidogo wa ziada, pesa zaidi ya tunavyohitaji, na fursa nyingi na kubwa kuliko zile tumekuwa nazo awali? Tutafanya je wakati itakuwa ni kama sio lazima kumtegemea Mungu saana kama kawaida? Tutamsahau Mungu na kuenda njia zetu? Mungu anaweza kutuaminia fanaka? Jiadae na ujipange sasa kufaulu  mtihani wa tabia na uendelee kuwa na faradhi.

*Ombi la leo*: Mungu, nataka kukutumikia siku zote za maisha yangu.nipe nguvu na uvumilivu ili nikae katika mkondo na nifike juu zaidi kwa anjili yako.Nitakapofaulu, sitakusahau, Bwana.Nitaendelea kuishi kwa faradhi yangu kwako na niendelee kuwa mdogo machoni mwangu mwenyewe.

*Maandiko ya leo*: Kumbukumbu la torati 8:10-14; nawe utakula ushibe, utamshukuru Bwana, Mungu wako, kwa nchi nzuri aliyokupa. Jihadhari, usije ukamsahau Bwana, Mungu wako, kwa kutozishika amri zzake, na hukumu zake, na sheria zake, ninazokuamuru leo. Angalia utakapokuwa umekula na kushiba, na kujenga nyumba nzuri na kukaa ndani yake; na makundi yako ya ng’ombe na kondoo yatakapoongezeka, na fedha yako na dhahabu yako itakapoongezeka, na kila kitu ulichonacho kitakapoongezeka, basi hapo moyo wako usiinuke, ukamsahau Bwana, Mungu wako, aliyekutoa nchi ya Misri, katika nyumba ya utumwa

## ***Watu wengine hushindwa na kukosa kujifunza chochote katika nyendo…janga gani hili.***

Sio hali tunazozipitia ila ni  pale tunapoelekea ambapo panajalisha sana. Hali za maisha zinaweza kutushusha moyo ama kutuelimisha……… ni uamuzi wetu. Hatuwezi wakati wote kuelewa pale tunapopitia lakini tuna amua jinsi tutakavyo enda.

Amua siku ya leo kwamba shinikizo na shida za maisha na pia makosa yako utayatumia yawe ni funzo kwako, ili kwamba kubatilisha kama huko hakutarudiwa tena usoni. Ujuzi mara nyingi ndio mwalimu bora zaidi, hata ujuzi mbaya. Jufunze kutokana na makosa yako.

*Ombi la leo*: Mpenzi Mungu, nitunukie hekima yakukubali makosa yangu kulingana na mtazamo wa kiungu. Tumia maisha yangu kunifunza mimi na wengine mafunzo

makuu kuhusu usoni mwetu. Nisamehe ambapo nimekukosea Wewe na unipeleke kwa siku zangu kuu.

*Masomo ya leo:* Zaburi 51:10 -12; ee Mungu, uniumbie moyo safi, uifanye upya roho iliyotulia ndani yangu.usinitenge na uso wako, wala roho yako mtakatifu usiniondolee. Unirudishie furaha ya wokovu wako; unitegemeze kwa roho ya wepesi.

## *Muondoko wa Mungu si ujuzi uliotengwa lakini umekusudiwa kudumu milele.*

Muondoko wa Mungu ulio wa ukweli, utaadhiri maisha yetu ya kibinafsi, kifamilia, na kijamii kwa karne zijazo. Hali ya kienyenji, nyakati chache za kusherehekea na/ama kuburudika, ingawa ni zakufurahisha sio lazima ziwe na mwongozo wa kweli wa Mungu. Mungu akitembea, watu na vitu hubadilika. Watu huanza kuishi maisha ya usawa, ambayo yanampendeza Mungu.

Mwondoko wa Mungu si ujuzi uliotengwa lakini umekusudiwa kudumu milele.Inaweza chukuwa miaka kabla ya kujua kama kweli tulikuwa na muondoko wa Mungu. Badala ya kubebwa na mawimbi ya maisha, siku hii juu na nyingine chini, kuishi maisha ya ujuzi huu wa kiroho na kuendelea kwa mwingine, sherehe hadi nyingine, karamu kwa karamu, muulize Mungu atembee kwa ukweli maishani mwako……….. mwondoko ambao utaendelea kwa zaidi ya saa moja, siku moja, ama juma moja. Imarisha maisha yako ya kikristo kila siku.

*Ombi la leo*: Mungu, nakuomba utembee maishani mwangu na njia itakayonibadilisha na kwamba kila siku nikue katika neema na kibali chako. Nipe maisha imara ya ukristo. Nitenganishe na hofu, mashaka na mfadhaiko. Wacha furaha iwe sehemu yangu na amani iwe tuzo kwangu. Nikuze niwe kama wewe. Nataka niishi maisha makuu kwa ajili Yako.

*Masomo ya leo*: Marko 4: 5,6,15,16; Nyingine zilianguka penye mawe pasipokuwa na udongo mwingi. Mbegu hizo ziliota mara kwa kuwa udongo haukuwa na kina. Jua lilipochomoza, zikachomeka; na kwa kuwa mizizi yake haikuwa na nguvu, zikanyauka. Watu wengine ni kama wale walio njiani ambapo mbegu zilianguka. Hawa hulisikia hilo neno lakini mara Shetani huja na kuliondoa neno hilo lililopandwa ndani yaolililipochomoza. Watu wengine ni kama zile mbegu zilizopandwa penye mawe. Mara tu wanapolisikia hilo neno hulipokea kwa furaha lakini haliwaingii na kuwa na mizizi ndani yao; huendelea kulizingatia kwa kitambo tu, na wakati taabu au udhalimu vinapotokea kwa sababu ya hilo neno mara wanakata tamaa.

## *Usiyatumie maisha yako yote ukipanda ngazi unapofika juu ugundue iliegemea jengo lisilofaa.*

Tumesikia ikisemekana ‘jambo la muhimu ni kudumisha jambo la maana liwe jambo la maana’. Jambo la maana ni lipi? Ni kazi; ni mali, ama labda mamlaka, utawala, ama kitu cha kujivunia? Kati ya haya hakuna kinachoweza kutosheleza hamu ya

nafsi. Kama fanaka hutosheleza kwa ukweli, basi watu kama Elvis Presley wangekuwa bado wanaishi kwa furaha.

Jambo la maana ni lipi? Kutafuta na kufuata mapenzi ya Mungu maishani mwako. Hakuna lingine la kuridhisha katika maisha haya ama maisha yajayo. Amani rohoni mwetu na furaha manyumbani mwetu ni matukio ya kuishi maisha yanayo mfurahisha Mungu. Muulize Mungu jinsi unavyoweza pata riziki, tengeneza maisha, na ufanye utofauti ukiwa ungali unaelekeza mtazamo wako kwa jambo la maana. Je, kuna kitu utapoteza?

*Ombi la leo*: Bwana, nataka kuishi maisha sio ya kukupendeza wewe pekee lakini yatakayonitosheleza mimi pia. Ningependa kuwa mtu ambaye amefaulu na niwe wa maana kwako na kwa mpango wako vile vile. Nionyeshe vile nitakavyofanya. Badilisha mtazamo wangu pahali unahitaji kubadilishwa. Nisaidie nione na nipange aula zangu.

*Maandiko ya leo*: Mathayo 16:26 Lakini mtu anayeyapoteza maisha yake kwa ajili yangu, atayapata. Je, mtu atafaidi nini akiupata utajiri wote wa ulimwengu na hali amepoteza maisha yake? Au, mtu atatoa kitu gani kiwe badala ya maisha yake?

1 Timotheo 6:17 Waamuru watu walio matajiri katika mambo ya maisha ya sasa, wasijivune, wasiweke tumaini lao katika mali isiyoweza kutegemewa; bali wamtegemee Mungu, ambaye kwa ukarimu hutupatia vitu vyote tuvifurahie.

Mathayo 6:33; Bali, zingatieni kwanza Ufalme wa Mungu na matakwa yake, na hayo mengine yote mtapewa kwa ziada.

## *Imani sio kutokubali shida ila haki yake yakuendelea*

Katika Mwanzo Mungu alipoona kitu ambacho hakikumpendeza na akataka kukibadilisha, alinena. Mungu aliweka kiwango cha mambo ambayo sasa tunayaelewa kama ' imani na kukiri' aliposema, 'wacha kuwe na nuru!' Mungu hakukataa kuwa kulikuwa na giza. Ili aweze kuleta mabadiliko kamili, Mungu aliviita vitu ambavyo havikuweko kana kwamba vilikuweko, na wala sio kinyume.

Wakristo wanahimizwa katika Agano Jipya kuwa kama Mungu na pia 'ita mambo hayo ambayo hayapo kana kwamba yapo'. Hatufai kutokubali milima ya shida ambazo tunakumbana nazo, lakini tunafaa kukataa haki yake yakuendelea pale tukinena kwa imani na tukiamuru milima ile iondoke. 'haiko pale' haitafaulu.

*Ombi la leo:* Baba, niwezeshe kukumbana na shida na hali za maisha ambazo hazinifurahishi na zinahitaji mabadiliko. Nipe imani ya kuamini na nguvu ya kutangaza kile ninachoamini ni mapenzi yako maishani mwangu. Nipe malaika walio na jukumu wakishughulikia matangazo yangu ya imani.

*Maandiko ya Leo*: Mwanzo 1:3; Mungu akasema, 'iwe nuru', ikawa nuru.

Warumi 4:17; Kama Maandiko Matakatifu yasemavyo: "Nimekuweka uwe baba wa mataifa mengi." Ahadi hiyo ni kweli mbele ya Mungu ambaye Abrahamu alimwamini--

Mungu ambaye huwapa wafu uzima, na kwa amri yake, vitu ambavyo havikuwa huwa.

Waebrania 10:23; Tushikilie imara tumaini lile tunalokiri, maana Mungu aliyefanya ahadi zake ni mwaminifu.

## ***Mara nyingi shida kuu tunazokutana nazo ni uamuzi mzito na ambao unatulazimu kuufanya.***

Labda wewe pekee ndiwe unaweza kufanya jambo kuhusu mambo hayo yanayokusumbua. Maishani, inatubidi tufanye uamuzi mkubwa mara kwa mara. Shida nyingi ambazo tunakutana nazo ziko katika sehemu za maisha ambazo tunajua zinahitaji kuangaliwa. Tukiyaachilia yenyewe, mambo mabaya hayatakuwa mema ila mabaya zaidi.

Maisha yanatulazimu kuchukua hatua ya usawa inayoleta utofauti. Nini kinachohitaji kubadilika katika maisha yako? Shida zako nyingi kiini chake ni nini? Utafanya nini kuihusu? Hata kama hautaki, utalazimika kufanya uamuzi mzito. Kama ni hivyo, uandike chini na uongee na Mungu. Atakusaidia kufanya uamuzi.

*Ombi la leo*: Mungu, ninajua kwamba imenifanya wakuajibika katika maisha yangu. Nipe macho ya kuona kiini cha yale mambo ambayo hunikera zaidi na unikirimie nguvu yakufanya jambo kuihusu kama ninaweza. Nipe neema ya kuwa imara na mwenye uamuzi nikiwa pia nabaki mpole, mwenye huruma na mtulivu.

*Maandiko ya leo*: Kumbukumbu la Torati 30:19; nazishihudia mbingu na nchi yenu leo, kuwa nimekuwekea mbele yako uzima na mauti, baraka na laana, basi, chagua uzima, ili uwe hai, wewe na uzao wako.

Warumi 14:12; Kwa hiyo, kila mmoja wetu atatoa hoja yake mbele ya Mungu.

Zaburi 18:35; Nawe umenipe ngao ya wokovu wako, mkono wako wa kuume umenitegemeza, na unyenyekevu wako umenikuza.

## ***Lazima tuanze pale tulipo ili tufike kule tunaenda, tutumie tulicho nacho kupata kile tunachotaka, na kujaribu tusichoweza ili kufaulu kwa yote.***

Kuna mtindo wa kipekee wa maisha. Mungu ametupa vitu vya kufanyia kazi ili tuweze kufaulu katika mapenzi yake na makusudi yake katika maisha yetu. Tena anatupa ndoto, maono, shauku kuu, na matumaini. Hivi vyote viko hapa ili kutia moto tuchukue tulicho nacho, tuanze pahali ambapo tupo na tufanye yote tunayoweza kufanya.

Wakati wote, sio vyema kungojea kumaliza kabla hata hatujaanza. Maisha hutupa fursa ambazo wakati mwingine huonekana kana kwamba haziwezekani, ilhali zinanenea ndoto mioyoni mwetu. Zaidi ya kutengeneza pesa tu, shauku la ndoto ya Mungu hunenea tamaa za nafsi zetu. Ndoto yako ya Mungu ni ipi? Unafanya nini kuihusu sasa?

_Ombi la Leo_: Kuamini kwangu, ni ndani Yako Mungu. Najua siwezi kutegemea uwezo wangu ulionipa ili nitimize mapenzi na makusudio Yako. Nisaidie kujua jambo la kufanya, wakati wa kulianza, na jinsi ya kuendelea. Siku zangu za usoni ni zako.

_Masomo ya leo_: 2 Wafalme 4:2; Elisha akamwambia, Nikufanye nini?' Niambie. Una kitu gani nyumbani? Akasema, 'mimi mjakazi wako sina kitu nyumbani ila chupa ya mafuta.'

Mathayo 14:17; Lakini wao wakamwambia, "Tunayo mikate mitano tu na samaki wawili."

Wafilipi 4:13; nayaweza mambo yote katika Yeye anitie nguvu.

Wafilipi 4:19; Na Mungu wangu atawajazeni na kile mnachohitaji kwa kadiri ya utajiri wake, katika utukufu ndani ya Kristo.

## ***Sio lazima tuharibu jambo moja ili tujenge lingine.***

Katika majira fulani na katika hali zingine za maisha, sisi hujikuta tukiwa kwa kipindi cha mageuzi. Mageuzi hutubadilisha kiasili, kiroho, ama kifilosofia kutoka mahali pamoja hadi pengine. Mageuzi yaweza kuwa mazito hata bila sisi kuharibu zaidi.

Ni sawa kufurahia jambo mpya. Sio lazima tuharibu lile zee ili tupate hili geni. Mageuzi mengine hayahitaji kuelezewa. Usikubali shaka zako ama za wale wamekuzunguka ziharibu kuhusika kwako kwa awali. Twaweza kufurahia tunakoelekea bila kukashifu pale ambapo tunatoka.

_Ombi la leo_; Baba, nifundishe njia ya usawa ambayo ina faida yakufanya ugeuzi maishani mwangu. Nataka kuwa na shukurani kwa yale umenitendea na yale unaendelea kunitendea pahali ambapo umeniweka. Bado ninafurahia na kukumbatia yale utakayonitendea, na pahali unaponielekeza. Nisaidie niiweke safari yangu katika mtazamo na ikupendeze Wewe.

_Maandiko ya leo_: Waefeso 4:29; Maneno mabaya hata yasisikike kamwe miongoni mwenu; kila mara maneno yenu yawe ya kufaa na ambayo hujenga na kuwasaidia wengine, ili yawaneemeshe wasikilizaji wenu.

Warumi 16:17; Ndugu zangu, nawasihi muwafichue wote wanaosababisha mafarakano na kuwafanya watu wengine waanguke, kinyume cha mafundisho mliyofundishwa. Jiepusheni na watu hao,

2 Timotheo 2:23; Epuka ubishi wa kijinga na kipumbavu; wajua kwamba hayo huleta magomvi.

## ***Shetani asipokufanya uwe mbaya, atajaribu kukupa shughuli***

Ni tamaa ya shetani kukufanya upunguze mwendo, akupoteze njia, ama kama itawezekana akutoe katika safari kabisa. Uwongo ni adui mkuu kwa sababu unandanganya sana. Watu waweza kuwa na shughuli, wakifanya kazi ya Bwana, wakiwa katika shughuli zao za maisha wakionekana kama wenye mazao mengi, kumbe hawana matunda yoyote yenye udhamana.

Shetani asipokufanya uwe mbaya, atajaribu kukupa shughuli. Kuwa na shughuli nyingi hadi ushindwe kuwasiliana na Mungu, familia, kanisa na jamii kwa njia ya usawa na ambayo ina maana, ni kuwa na shughuli zaidi. Jikague mwenyewe. Je, una shughuli nyingi sana hata haufurahii baraka ambazo Mungu amekukirimia? Kama ni hivyo, angalia ni mambo yapi utakoma kufanya bila kugusa ya Mungu na ya familia.

*Ombi la leo:* Mungu nisaidie nichunguze jinsi ninatumia wakati wangu, majukumu yangu ya haja kubwa, na mazao ninayopata. Nataka niwe zaidi ya mshumaa uwakao pande zote. Nipe mpango niweke maisha yangu kwa utaratibu na umoja na makusudio Yako. Nisaidie Bwana kufurahia baraka unazopeana.

*Maandiko ya leo*: Luka 10: 39-42; Martha alikuwa na dada yake aitwaye Maria; huyu aliketi karibu na Yesu akisikiliza mafundisho yake. Lakini Martha alikuwa anashughulika na mambo mengi. Basi, akamwendea Yesu, akamwambia, "Bwana, hivi hujali kwamba dada yangu ameniacha nishughulike peke yangu? Mwambie basi, anisaidie." Lakini Bwana akamjibu, "Martha, Martha, unahangaika na kusumbuka kwa mambo mengi. Kitu kimoja tu ni muhimu. Maria amechagua kitu bora zaidi ambacho hakuna mtu atakayemnyag`anya."

Zaburi 46:10; Acheni, mjue ya kuwa Mimi ni Mungu…

## ***Maombi sio kiungo cha maisha tunachomwagilia juu ya mipango yetu ili tuifanye ionje kiungu… maombi ndiyo kiungo haswa kinachotupa sisi utaratibu wa kutengeneza maisha yetu***

Zaidi ya ukawaida wa kutafuta baraka za Mungu katika harakati zetu, maombi ni njia ya mawasiliano tunayoifurahia ambayo hufungua mlango wa uhusiano na Mungu. Maombi ni njia Mungu hutumia kutuma jumbe zake kwa moyo na mawazo yetu. Tunapoomba, Mungu hunena na nafsi zetu na tunajiwachilia wakati mwingine bila ufahamu wetu. Yeye hutupa hisia zingine za mwelekeo na majibu ya maswali yetu.

Maombi sio kiungo cha maisha tunachomwagilia juu ya mipango yetu ili tuifanye ionje kiungu… maombi ndiyo kiungo haswa kinachotupa sisi utaratibu wa kutengeneza maisha yetu. Badala ya kujaribu kupata baraka za Mungu kwa yale tunayotenda, labda tungetumia wakati tujue kile anachofanya Mungu na tujishughulishe na mpango wake.

_Ombi la leo_: Baba najua una mpango kamili, kusudi na mapenzi katika maisha yangu. Nakuomba uninenee na unifafanulie mpango kamili. Sitaki nikutumie kana kwamba mimi ndiye muhimu zaidi ama mwenye hekima zaidi katika uhusiano huu. Nionyeshe mapenzi Yako. Najua tayari imebarikiwa.

_Maandiko ya leo_: Mithali 3:5-8; Mtumaini Bwana kwa moyo wako wote, wala usitegemee akili zako mwenyewe; katika njia zako zote, mkiri Yeye, naye atayanyosha mapito yako. Usiwe mwenye hekima machoni pako; mche Bwana, ukajiepushe na uovu. Itakuwa afya mwilini pako, na mafuta mifupani mwako.

## ***Mitihani minne maishani: wa kwanza: mtihani wa bonde***

Mabonde ni mahali pa chini maishani. Wakati mwingine, sote hujipata pahali pale pa chini, tukijaribiwa kufadhaika, kujiondoa, kukubali hisia za kushindwa na fursa za kukoma. Bondeni sio pahali pazuri pa kufanyia uamuzi. Mtazamo wetu hudhibitishwa na mambo ambayo yanatuzunguka na hivyo maono yetu hudunishwa.

Usiogope kuwa utawachwa wakati uko kwenye bonde. Pambana na hisia za ukiwa chini na ushinde majaribu ya kuwachilia malengo yako unapojisikia mdhaifu. Kumbuka, Mungu yu pamoja nawe na atakusaidia kubadilisha kinachohitaji kubadilishwa ndani ya bonde lako.

_Ombi la leo_: Bwana, nisaidie leo niwe imara na mwenye nguvu nitakapo pitia mtihani wangu wa bonde katika maisha yangu. Najua naweza kukuamini Wewe na kwamba Wewe una tabia ya ukweli na unatamani kunionyesha nguvu zako. Nisaidie nitembee pamoja na wengine na niwatie moyo wakati wanapitia mabonde yao pia.

_Maandiko ya leo_: Zaburi 23:4-6; naam, nijapopita kati ya bonde la uvuli wa mauti, sitaogopa mabaya; kwa maana Wewe upo pamoja nami, gongo Lako na fimbo Yako vya nifariji. Waadaa meza mbele yangu, machoni pa watesi wangu.umenipaka mafuta kichwani pangu, na kikombe changu kinafurika. Hakika wema na fadhili zitanifuata siku zote za maisha yangu; nami nitakaa nyumbani mwa Bwana milele

## ***Mitihani minne maishani: wa pili: Mtihani wa kilele cha milima***

Katika milima ya maisha, karibu na nyota, na pepo safi zikileta raha na siku za mabonde zikiwa nyuma yetu, maono yetu yaweza kuoneka kama ni makuu. Hizi ni nyakati tunazohitaji kukumbushwa uamuzi wowote mpya tunaofanya juu ya mlima huu, itatupatia fursa nyingi za upanuzi. Tunaweza kukwea juu zaidi, au kuteremka chini tena kupitia njia tofauti ama pia katika bonde lingine la mng’ang’ano wa maisha.

Tunakuja milimani kuhuishwa, kuona fanaka zetu zilizopita na kukumbatia changa moto zingine. Mtihani wa mlima ni huu: utakumbatia changa moto nyingine na uhatarishe kukumbana na bonde ama utakomea hapo?

*Ombi la leo*: Baba, nisaidie kubakia mwadilifu na mwenye kukolea katika uhusiano wangu na Wewe, hasa wakati nitakapokuwa ninapitia juu ya milima maishani mwangu. Nipe moyo wa kukufuata kila wakati. Nipe maono mapya na ujasiri unaostahili kuendelea katika maisha.

*Maandiko ya leo*: Joshua 14;10-12; 'Sasa basi, angalia, Yeye Bwana ameniweka hai, kama alivyosema miaka hii arobaine na mitano tangu wakati huo Bwana alipomwambia Bwana neno hilo, wakati Israeli waliokuwa wakienenda barani, na sasa tazama, hivi leo nimepata miaka themanini na mitano umri wangu.hata sasa mimi nina nguvu zangu hivi leo kama ilivyokuwa siku hiyo ya Musa aliyonituma; kama nguvu zangu zilivyokuwa wakati huo, na nguvu zangu ndivyo zilivyo sasa, kwa vita, na kwa kutoka nje na kwa kuingia ndani. Basi sasa unipe mlima huu, ambao Bwana alinena habari zake siku hiyo; kwani wewe ulisikia siku hiyo Waanaki walivyokuwa huko, na miji ilivyokuwa mikubwa yenye boma; yumkini yeye Bwana atakuwa pamoja nami, nami nitawafukuza watoke nje, kama Bwana alivyonena.'

Wafilipi 4; 13; nayaweza mambo yote katika Yeye anitie nguvu.

## *Mitihani minne maishani: wa tatu: mtihani wa kusubiri*

Mkulima hupanda mbegu yake kwa mchanga na kisha akaifunika. Ingawa msimu ujao atatengeneza mchanga na mmea huu mchanga akingojea kwa subira matunda ya kazi yake yaweze kutokea. Kupitia ujuzi, mkulima amejifunza kutarajia hata siku zile zinaoonekana ni kama hakuna dhibitisho. Kanuni hii ni ya ukweli katika maeneo mengine mengi maishani. Sisi hupanda wakati wetu, maombi yetu, juhudi zetu ambazo tumeidhamini, na wakati mwingine tunajaribiwa kuona kama haya yote haina maana. Huu ndio mtihani wa kungojea. Kama wakristo tunajua kwamba Mungu hafurahii wakati tunakosa subira lakini na wakati wake mwenyewe. Muamini Mungu wakati wewe umeyafanya yote ambayo ungeweza na umngojee Yeye… huja wakati unao faa.

*Ombi la leo*: Ewe Baba, nisaidie ninapohitaji subira. Nitunukie neema Yako spesheli ili nipite mtihani wa subira. Najua wewe ni wa haki na wakati wako ndio bora zaidi. Ahsante kwa kuwa na subira juu yangu.

*Maandiko ya leo*: Yakobo 5:7; Basi, ndugu zangu, muwe na subira mpaka Bwana atakapokuja. Tazameni mkulima anavyongoja kwa subira mimea yake itoe mavuno mazuri. Yeye hungojea kwa subira mvua za masika na za vuli.

Zaburi 27:14; umngoje Bwana, uwe hodari; upige moyo konde, naam, umngoje Bwana

## *Mitihani minne maishani: Wa nne: mtihani wa kumaliza*

Mambo huanza na mambo huisha. Ni hakikisho la maisha. Kwa mfano, kijana wa kiume ambaye amechumbiana ili afanye ndoa. Siku ambayo atafanya agano hili na bibi arusi, maisha yake ya uhuni yatakwisha. Ni ukurasa ambao uliokwisha na, amini usiamini, kutakuwa na mtihani.

Kuna wakati maishani ambapo sisi sote huwacha kuangalia kwa umakini mambo ambayo hapo awali yalituhusu, kwa vile yako nyuma yetu na hayatulazimu wala kustahili umakini wetu. Inaweza kutokea kwa kustaafu, kubadilishwa ama kifo cha mkeo/mumeo. Katika nyakati hizi, ni muhimu kukubali hatimu za maisha, weka yaliyopita kwa mtazamo unaofaa, kumbatia siku za usoni, na uwe tayari mtihani unao fuata, ambao ni lazima uje.

*Ombi la leo:* Baba, nisaidie kumaliza safari yangu maishani kwa imani. Wakati jukumu moja linapo kamilika na siku mpya ama mwaliko mpya unaanza, nisaidie kukumbatia yasiyojulikana kwa ujasiri nikijua ya kwamba uko nami kila hatua.

*Maandiko ya leo*: Wafilipi 3:13-14; ama kweli, ndugu zangu, sidhani kuwa mmekwisha pata tuzo hilo, lakini jambo moja nafanya; nayasahau yale yaliyopita na kufanya bidii kuyazingatia yale yaliyo mbele. Basi, nimo mbioni kuelekea lengo langu, ili nipate lile tuzo ambalo ni mwito wa Mungu kwa maisha ya juu kwa njia ya Kristo Yesu.

Isaya 43:18-19; Msiyakumbuke mambo ya kwanza, wala msiyatafakari mambo ya zamani. Tazama, ninatenda neno jipya, sasa litachipuka, je! Hamtalijua sasa? Nitafanya njia hata jangwani, na mito ya maji nyikani.

## *Mara kwa mara tunawekewa kiwango na kutokuwa na hiari kuchukua mwelekeo*

Watu wengi Marekani wamelelewa na hali ya kujitegemea wenyewe. Wao huona vigumu kunyenyekea na kukubaliana na wazo au kauli la mwingine. Wanapo ulizwa kuhusika kwa kitu wasichoweza kutawala, wao hupata changamoto zaidi. Kujiunga na jeshi mpaka kuhusika na majukumu yalio pangwa ya kijamii, watu wengi hupenda kuwa na mamlaka hata kubla hawajausishwa.

Hii pia inaleta changamoto ya kipekee kwa wengine, katika kujitolea kwa Kristo. Tayari wanamkubali kama Mwokozi, lakini kwa ulegevu kama Bwana. Hata hivyo hamna nafasi ya zaidi ya mtu moja katika enzi ya maisha yako. Ni wewe ama ni yeye?

*Ombi la leo*: Baba mungu, nakuomba unisaidie kuwacha kujitawala maisha yangu na kupatia uamuzi wangu kwake Yesu, Bwana wangu na Mwokozi. Nifunze njia yako nami nitafuata.

*Maandiko ya leo:* Matendo ya Mitume 2:36 "Watu wote wa Israeli wanapaswa kufahamu kwa hakika kwamba huyo Yesu mliyemsulubisha ninyi, ndiye huyo ambaye Mungu amemfanya kuwa Bwana na Kristo

Yohana mtakatifu 14:15"Mkinipenda mtazishika amri zangu.

Waraka wa Yakobo 4:7 Basi, jiwekeni chini ya Mungu; mpingeni Ibilisi naye atawakimbieni.